

**CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO (SUA)**

**MOROGORO**



**MKATABA WA HALI BORA**

**MEI, 2023**

PRESIDENT'S OFFICE  
PUBLIC SERVICE MANAGEMENT  
P.O.Box 670  
DODOMA

## YALIYOMO

<b>YALIYOMO .....</b>	i
<b>VIFUPISHO .....</b>	iii
<b>DIBAJI .....</b>	iv
<b>SHUKRANI .....</b>	v
<b>MAANA YA MANENO KATIKA MKATABA HUU .....</b>	vi
<b>SEHEMU YA KWANZA .....</b>	1
<b>UTANGULIZI .....</b>	1
1.1 Msingi .....	1
1.2 Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi Kazini.....	1
1.3 Dira na Dhima ya Chuo na Malengo ya Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi.....	2
1.3.1 Dira ya Chuo.....	2
<b>SEHEMU YA PILI .....</b>	3
<b>UTAMBUZI NA UFAFANUZI .....</b>	3
2.6. Makubaliano .....	3
2.7 Kuanza na Kudumu kwa Mkataba .....	3
<b>SEHEMU YA TATU .....</b>	5
<b>NIDHAMU, MWENENDO WA MASHAURI NA UTATUZI WA MIGOGORO .....</b>	5
<b>SEHEMU YA NNE .....</b>	6
<b>UFUTWAJI, UPUNGUZWAJI NA KUONDOLEWA KAZINI WAFANYAKAZI KWA MISINGI MBALIMBALI .....</b>	6
<b>SEHEMU YA TANO.....</b>	7
<b>LIKIZO .....</b>	7
5.1 Likizo ya Mwaka .....	7
5.2 Likizo Bila Malipo ya Kisheria .....	7
5.3 Likizo ya Ugonjwa.....	7
5.4 Likizo ya Uzazi .....	7
5.5 Likizo Maalum .....	7
<b>SEHEMU YA SITA.....</b>	8
<b>BURUDANI, MATIBABU, POSHO NA STAHILI MBALIMBALI ZA WAFANYAKAZI .....</b>	8
6.2 Matibabu na Afya ya Mtumishi .....	9
6.3 Posho na Stahili Mbalimbali za Wafanyakazi.....	9
6.4 Mazingira Hatarishi.....	9
6.5 Posho ya Saa za Ziada.....	9
6.6 Marupurupu ya Wastaifu .....	9

6.7 Mavazi Rasmi na Vifaa vya Kujikinga Kazini.....	10
6.8 Zawadi kwa Wafanyakazi Bora.....	10
6.9 Elimu kwa Wafanyakazi.....	10
6.10 Ushughulikiwaji wa Vifo .....	11
6.11 Uundaji wa Vyama vya Ushirika.....	11
<b>SEHEMU YA SABA.....</b>	<b>12</b>
VIMA VYA MISAHARA NA NYONGEZA.....	12
<b>SEHEMU YA NANE.....</b>	<b>13</b>
MAPATO YATAKAYOWEZESHA KUTEKELEZA MKATABA.....	13
<b>SEHEMU YA TISA.....</b>	<b>14</b>
HITIMISHO .....	14
<b>SEHEMU YA KUMI.....</b>	<b>15</b>
<b>REJEA .....</b>	<b>15</b>

## **VIFUPISHO**

COTWUT	Tanzania Communication and Transport Workers Union (Chama cha Wafanyakazi wa Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania)
NBC (T)	National Bank of Commerce (Tanzania)
RAAWU	Researchers, Academicians and Allied Workers Union
SUA	Sokoine University of Agriculture
TAFIRI	Tanzania Fisheries Research Institute
TPB	Tanzania Postal Bank
TUICO	Tanzania Union of Industrial and Commercial Workers
VETA	Vocational Education and Training Authority

## DIBAJI

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia, Habari na Utafiti (RAAWU) Tawi la SUA, walianzisha mchakato wa kupata Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini mnamo mwaka 2008.

Mkataba huu unalenga kuweka mazingira bora ya kufanya kazi ili kuongeza ufanisi na tija, kuboresha maslahi na wakati huo huo kutoa huduma bora kwa Wadau wa Chuo wakiwemo wanafunzi, wakulima, wafugaji na wananchi kwa ujumla wao wanaofika chuoni kupata huduma mbalimbali zitolewazo na Chuo.

Dhumuni kubwa la kuandaa Mkataba huu ni kuboresha utendaji na utoaji huduma wa Chuo kwa jamii, msisitizo ukiwa ni kuwahudumia Wadau wa Chuo kulingana na mahitaji na matarajio yao. Hii inamaanisha kuwa Chuo kinatakiwa kuwa na ufanisi zaidi kwa kutoa huduma bora zaidi kulingana na mahitaji na matarajio ya wadau. Aidha, inatarajiwa kwamba wafanyakazi watakuwa wasikivu, watatumia ubunifu zaidi kwa Wadau wa Chuo na kuwajibika ipasavyo ili kuleta tija. Kupitia utekelezaji wa Mkataba huu, mazingira ya kazi na maslahi ya wafanyakazi yataboreshwa na kwamba tija inayotarajiwa itapatikana, na hivyo kukiwezesha Chuo kutimiza ndoto yake ya kuwa Mwajiri bora nchini.

Inashauriwa kuwa ni vyema wahusika kwa maana ya watumiaji wa Mkataba huu, akiwemo Mwajiri na Mfanyakazi wakaongeza uelewa kwa kusoma miongozo mbalimbali ili kurahisisha utekelezaji wa Mkataba huu wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini.

## SHUKRANI

Utayarishaji wa Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini umefanikishwa kuitia juhudii kubwa za Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kwa kushirikiana na Chama cha Wafanyakazi (RAAWU SUA) ambacho ndicho Wakala Maalum wa Majadiliano.

Menejimenti ya SUA pamoja na viongozi wa RAAWU Taifa na RAAWU Tawi la SUA walifanya kazi bila kuchoka katika kuratibu mchakato mzima uliowezesha kuandaliwa kwa Mkataba huu.

Mchakato wa utayarishaji wa Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini, umeendeshwa kwa kushirikiana na Wadau kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali na watu Binafsi. Hivyo inatarajiwa kwamba kuwa Mkataba huu utawanufaisha Wafanyakazi na Mwajiri wao.

Shukrani za pekee ziende kwa Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) na Halmashauri ya RAAWU Tawi la SUA kwa uwezeshaji na ushirikiano waliooutoa kwa pamoja wakati wa kuandaa Mkataba huu. Mchango wao ulisaidia kuhakikisha ubora wa Mkataba

Shukrani za dhati pia ziwaendee Wajumbe wa Baraza Kuu la Wafanyakazi la SUA kwa kuweka msisitizo na kuona kwamba Mkataba unakamilika. Aidha, maoni yao yalisaidia sana uandaaji wa Mkataba huu.

Kikosi Kazi kinatoa shukrani kwa wadau mbalimbali waliotoa michango yao katika kufanikisha uandaji wa Mkataba huu. Wadau hao ni pamoja na VETA na TPB Plc. Kwa kuwa siyo rahisi kutaja wadau wote mmoja mmoja, Menejimenti ya SUA na RAAWU Tawi la SUA wanatoa shukrani za pekee kwa Wafanyakazi na Wataalam mbali mbali walioshiriki katika kutoa taarifa zilizowezesha Mkataba huu uonekane kama ulivyo sasa.

## MAANA YA MANENO KATIKA MKATABA HUU

### Baraza la Chuo

Chombo huru cha uwakilishi kilichoundwa kwa mujibu wa wa sheria kusimamia sera pamoja na uendeshaji wa Chuo ili kuleta ufanisi katika maendeleo yake, ikiwa ni pamoja na masuala yanayohusu maendeleo ya Chuo kwa ujumla wake, changamoto zinazokikabili na mipango ya kukiimarisha kwa masuala ya kitaaluma na ki miundombinu.

### Baraza la Kuu la Wafanyakazi

Ni chombo kilichoundwa kisheria chenye kuwashirikisha wafanyakazi katika masuala mbalimbali sehemu za kazi kwa lengo la kutoa maoni ya namna bora ya kuinua ufanisi wa kazi, mahusiano mema na kupendekeza namna ya kutatua changamoto za Chuo

### Mwajiri

Baraza la Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)

### Chama

Idadi ya wafanyakazi kuanzia kumi walioungana pamoja kwa lengo; ikiwa kwa lengo hilo tu au kwa malengo mengine, la kuratibu mahusiano katika wafanyakazii na waajiri wao au chama cha waajiri ambako waajiri wamejiunga

### Wadaawa

Pande mbili za Mkataba

### Mkataba

Suala lolote la kikazi lilioandikwa na kuingiwa makubaliano baina ya Chama cha Wafanyakazi kilichosajiliwa na ambacho ni Wakala wa Majadiliano mahala pa kazi na Mwajiri au Chama cha Waajiri kilichosajiliwa.

### Mwajiriwa

Mwajiriwa ni mtu anayehusika na ajira inayoendeshwa na Mwajiri. Ajira inahusisha waajiriwa wa kudumu, waajiriwa wa muda, Meneja, Mkurugenzi, na vibarua. Waajiriwa wanaweza kuajiriwa na Mwajiri mmoja au zaidi (ajira ya msingi na ya ziada)

### Mfanyakazi

Mfanyakazi wa Chuo ye yeyote aliye na ajira ya kudumu na wale walioko katika mkataba maalum ya ajira au ajira za kazi maalum

### Familia ya Mfanyakazi

Kwa mujibu wa Mkataba huu ina maana kuwa: (i) Mke/Mume lakini ni Mume/Mke mmoja tu anayetambulika kisheria na Mwajiri (ii) Mtoto/Watoto: Ni yule/wale mwenye/wenye umri usiozidi miaka 18, na awe amesajiliwa/wamesajiliwa kisheria na

ambaye/ambao anamtegemea/wanamtegemea mahitaji yake/yao kutoka kwa Mfanyakazi, (iii) Wazazi wa mfanyakazi ni baba mzazi na mama mzazi.

### Taasisi

Katika mkataba huu ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA).

Chuo Kikuu  
Mnazi ya Taasisi  
Mnazi ya Kilimo

Mnazi ya Kilimo  
Mnazi ya Taasisi  
Mnazi ya Kilimo

## SEHEMU YA KWANZA UTANGULIZI

### 1.1 Msingi

Sisi, **Menejimenti ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA)** tujulikanao hapa kama "Mwajiri" na Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, **Sayansi, Teknolojia, Habari na Ufundi Stadi Tanzania (RAAWU- SUA)** tujulikanao hapa kama "Chama cha Wafanyakazi" na kwa hiari yetu na katika hali ya maelewano, tumefikia makubaliano katika masuala yaliyomo kwenye kumbukumbu hii, ambayo yanaweka utambuzi na Hali Bora zaidi za kazi, kwa wafanyakazi walioajiriwa na Taasisi hii.

Sura hii inaeleza nini maana ya Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini, dira na dhima ya Chuo pamoja na malengo ya Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini. Aidha, mapitio ya Mkataba huu yanatakiwa kufanyika kwa makubaliano ya pande zote mbili za Mkataba.

### 1.2 Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi Kazini

Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini ni makubaliano ya kimaandishi kati ya Mwajiri na Chama cha Wafanyakazi ambacho ni Wakala wa Majadiliano (Exclusive Bargaining Agent). Mkataba huu unaelezea huduma zinazotolewa na Chuo, majukumu na wajibu wa Mfanyakazi wa Chuo katika kutoa huduma hizo.

Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini, ni mkataba kati ya pande mbili; upande mmoja ni Mwajiri ambaye ni CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA KILIMO kilichoanzishwa na kinachoendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyuo Vikuu Na.7 ya mwaka 2005 pamoja na Hati Idhini ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ya mwaka 2007, na Chama cha Wafanyakazi ambacho ni Wakala Maalum wa Majadiliano kijulikanacho kama Chama cha Wafanyakazi wa Taasisi za Elimu ya Juu, Sayansi, Teknolojia, Habari na Utafiti (RAAWU) kilichosajiliwa chini ya Sheria Na.6 ya mwaka 2004 ya Vyama vya Wafanyakazi kwa upande mwingine.

Mkataba huu unalenga kuweka mazingira bora ya kufanya kazi ili kuongeza ufanisi na tija sehemu ya kazi, na wakati huo huo kutoa motisha kwa wafanyakazi. Mkataba huu ni wa hiari na utatumika kwa miaka mitatu kuanzia tarehe ya kuidhinishwa kwake. Iwapo itatokea haja ya kufanya mabadiliko, taarifa ya miezi mitatu itolewe kwa Wadaawa wa Mkataba huu.

Kwa ujumla Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini umetayarishwa kwa ushirikiano, majadiliano na makubaliano kati ya Chama cha Wafanyakazi (RAAWU Tawi la SUA) ambacho ni Wakala Maalum wa Majadiliano na Mwajiri. Kwa kawaida Mkataba huo utabdalika kufuatana na makubaliano ya pande zote mbili za Wadaawa.

Mapitio yanaweza kufanyika kila baada ya muda uliopangwa au kutokana na tukio fulani. Katika kufanya mapitio Mwajiri na Chama kinatakiwa kushirikiana na kukubaliana tena. Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi Kazini unasisitiza mawasiliano na mshikamano kwa pande mbili.

Aidha, pale ambapo Mkataba huu haukutoa maelekezo ye yeyote, zitazingatiwa Sheria za Kazi (Sheria ya Ajira na Mahusiano ya Kazini Na.6 na Sheria ya Taasisi

za Kazi Na.7, zote za mwaka 2004; Sheria ya Utumishi wa Umma ya Mwaka 2019 na Kanuni zake za mwaka 2022, Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009 na Miongozo mbalimbali ya Serikali inayosimamia Utumishi wa Umma).

### **1.3 Dira na Dhima ya Chuo na Malengo ya Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi**

#### **1.3.1 Dira ya Chuo**

Ni kuwa Chuo kinachoongoza kutoa elimu bora na ujuzi kwenye Taaluma za Kilimo na Sayansi huishi.

#### **1.3.2 Dhima ya Chuo**

Ni kuleta maendeleo kwenye Kilimo, Maliasili na Sekta huishi kuupitia Mafunzo, Tafiti na Utoaji Huduma.

#### **1.3.3 Malengo ya Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi Kazini**

Mkataba wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini umetengenezwa baina ya Chama cha Wafanyakazi RAAWU Tawi la SUA ambacho ni Wakala wa Majadiliano na SUA ili kutimiza malengo yafuatayo:

- (i) Kuwafanya Wafanyakazi kuwa na mtazamo wa kuiwekea malengo katika utekelezaji wa majukumu yao, kama ilivyo katika Mfumo wa Wazi wa Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS);
- (ii) Kuboresha maslahi ya wafanyakazi ili tija inayotarajiwa ipatikane;
- (iii) Kuboresha ongezeko la maslahi ya wafanyakazi wakati wa kukoma ajira;
- (iv) Kuboresha mazingira ya kazi, usalama wa Chuo na rasilimali zake ikiwemo rasilimali watu yatokeapo mabadiliko yoyote;
- (v) Kuvutia watu wenye elimu, ujuzi, uzalendo na uwezo mkubwa wa kazi kujinga na Chuo na hatimaye kuongeza tija na ufanisi; na
- (vi) Kuhakikisha kuwa kila Mfanyakazi ananufaika kulingana na uwezo wa Mwajiri na kuzingatia Miongozo ya Serikali.

**SEHEMU YA PILI**  
**UTAMBUZI NA UFAFANUZI**

- 2.1** (a) CHAMA kinatambua Serikali kuitia Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma kwamba BARAZA la Chuo ndiye MWAJIRI hapa chuoni ambaye anaajiri wafanyakazi ambao mionganoni mwao ni wanachama wake.
- (b) MWAJIRI anatambua kwamba kwa sasa, RAAWU ndicho Chama pekee cha Wafanyakazi ambacho ni Wakala Maalum wa Majadiliano katika sehemu ya kazi kwa kipindi cha Mkataba huu.
- 2.2** Mazungumzo na majadiliano kati ya CHAMA na MWAJIRI yawe yanafanyika katika hali ya Uwakilishi na Mamlaka. Hii ina maana kwamba, pande zote mbili ziwe tayari kuzungumza, kujadiliana na kufikia maamuzi katika kutatua changamoto za Wafanyakazi wanaohusika na Mkataba huu.
- 2.3** Utekelezaji wa maamuzi yaliyofikiwa kati ya MWAJIRI na CHAMA utawekwa katika maandishi, na kila upande kuwa na nakala ya maamuzi
- 2.4** MWAJIRI na CHAMA wanatambua majukumu ya pande zote mbili ili kuleta mahusiano bora na ushirikiano wenye tija mahala pa kazi.
- 2.5** (a) CHAMA kitafanya juhudzi za makusudi kuwaelimisha na kuendelea kuwahamasisha wafanyakazi kuijunga nacho ili kutimiza matakwa ya kisheria ya kuendelea kuwa Wakala.  
(b) MWAJIRI atatoa ushirikiano kwenye vipengele vya Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Chuo na Serikali inayosimamia Utumishi wa Umma wakati Chama kikitekeleza majukumu yake.

**2.6. Makubaliano**

**KWA HIARI YETU NA MAELEWANO, SISI RAAWU NA MENEJIMENTI YA SUA  
TUMEFIKIA MAKUBALIANO KATIKA MASUALA MBALIMBALI YALIYOMO  
KATIKA MKATABA HUU AMBAYO YANAWEKA BAYANA HALI BORA ZAIDI  
YA WAFANYAKAZI KAZINI**

**2.7 Kuanza na Kudumu kwa Mkataba**

- 2.7.1** Pande zote mbili katika Mkataba huu, tunakubaliana kwamba Mkataba huu uanze kutumika tarehe ambayo itathibitishwa na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR-MUUUB) na kudumu kwa miezi thelethini na sita (36).
- 2.7.2** Upande wowote utakaokusudia kufuta, kuongeza, kupunguza au kurekebisha kifungu chochote katika Mkataba huu unaweza kufanya hivyo kwa kuushirikisha

kwanza na kuupa taarifa ya muda usiopungua mwezi mmoja upande wa pili na kuelezea sababu za makusudio hayo ili wakubaliane.

- 2.7.3** Mkataba huu utaendelea kuheshimiwa hata baada ya muda uliowekwa katika kifungu 2.7.1 cha ibara hii, iwapo hapatakuwepo na upande utakaota taarifa kwa upande mwagine kwa makusudio ya kutengeneza upya au kuboresha.

## **SEHEMU YA TATU**

### **NIDHAMU, MWENENDO WA MASHAURI NA UTATUZI WA MIGOGORO**

- 3.1** Iwapo wakati wa Majadiliano baina ya pande zote mbili itashindikana kabisa kufikia muafaka, upande wowote una haki ya kuwasilisha mgogoro huo kwenye Mamlaka za Ndani kabla ya hatua ya kuupeleka kwenye Mamlaka nje ya Chuo. Migogoro hiyo ni kutolewana kati ya Mwajiri na Mfanyakazi, Mfanyakazi na Mfanyakazi au Chama cha Wafanyakazi na Mwajiri.
- 3.2** Migogoro na mashauri yote yanayohusu nidhamu kazini, itashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma na Miongozo mbalimbali ya Serikali inayosimamia Utumishi wa Umma.
- 3.3** Mwajiri na RAAWU watahakikisha kwamba haki inatendeka katika kushughulikia migogoro ya Wafanyakazi na kuhakikisha migogoro haitokei mahala pa kazi.

## **SEHEMU YA NNE**

### **UFUTWAJI, UPUNGUZWAJI NA KUONDOLEWA KAZINI WAFANYAKAZI KWA MISINGI MBALIMBALI**

- 4.1** Mwajiri na CHAMA wanakubaliana kwamba watafanya majadiliano ya namna bora ya kutekeleza iwapo kutatokea umuhimu wa kufuta, kupunguza na au kuondolewa kazini wafanyakazi.

## **SEHEMU YA TANO**

### **LIKIZO**

MWAJIRI na CHAMA kwa pamoja wanatambua kwamba, masuala yote ya likizo kwa Wafanyakazi yatashughulikiwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Miongozo ya Serikali.

#### **5.1 Likizo ya Mwaka na Gharama zake**

Likizo hii itashughulikiwa kwa Mujibu wa Kanuni H.1-5 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009, na pia Na. 6.1.1 ya Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini ya Mwaka 2004. Utaratibu wa malipo ya likizo utazingatia Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma na Miongozo ya Serikali ya Utumishi wa Umma, ambapo mfanyakazi anapaswa kulipwa likizo moja kila baada ya miaka miwili ya likizo.

#### **5.2 Likizo ya Bila Malipo ya Kisheria**

**5.2.1** Likizo ya Bila ya Malipo itaombwa na Mtumishi katika Ofisi ya Katibu Mkuu Utumishi kuititia kwa Mwajiri wake. Mtumishi atapaswa kusubiri ruhusa kutoka ofisi hiyo kabla ya kuondoka kwa ajili ya likizo hiyo. Katibu Mkuu Utumishi baada ya kujiridhisha kuwa likizo hiyo ni kwa Manufaa ya Ofisi ya Umma itaidhinisha likizo hiyo.

**5.2.2** Likizo hii itashughulikiwa kwa mujibu wa Kanuni H. 19 ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za Mwaka 2009.

#### **5.3 Likizo ya Ugonjwa**

Pande zote za Mkataba huu zinakubaliana kwamba, mfanyakazi atapatiwa Likizo ya Ugonjwa yenye malipo endapo atapatwa na maradhi akiwa katika utumishi. Aidha, likizo hii itaidhinishwa kwa Miongozo wa Kanuni K.13 (1) - (5) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

#### **5.4 Likizo ya Uzazi**

Likizo ya Uzazi itatolewa kwa kuzingatia Kanuni H.12 (1) - (7) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

#### **5.5 Likizo Maalum**

Pande zote mbili zinakubaliana kuwa, kutakuwa na Likizo Maalum ambazo Mfanyakazi atapewa. Likizo hizo zitaidhinishwa kwa mujibu wa Kanuni H.14 (1) - (3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009.

## SEHEMU YA SITA

### BURUDANI, MATIBABU, POSHO NA STAHIKI MBALIMBALI ZA WAFANYAKAZI

Watumishi wa Umma/Chuo ni rasilimali na nguzo muhimu katika kufikia malengo na kuleta ufanisi katika Taasisi na nchi kwa ujumla. Ni wajibu wa Mfanyakazi kuchangia katika kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa na Mwajiri wake, kwa kiwango cha juu cha uaminifu, uadilifu, ukarimu na upole, ikiwa ni pamoja na kutafuta na kuchukua fursa zinazojitokeza, kuendeleza stadi na ujuzi wao wa kazi.

Mwajiri anao wajibu wa kuweka mazingira wezeshi kwa watumishi kutekeleza wajibu wao ikiwemo kuboresha afya zao, uwepo wa usalama mahala pa kazi na kuwalipa stahiki zao kwa wakati, kutambua na kuthamini michango yao ya kiutumishi na kuthamini utu wao.

Burudani ni shughuli ambazo mtu anazifanya kwa hiari yake ili kurudisilia nguvu, akili na ari alizotumia wakati wa kufanya kazi. Aidha, burudani humfariji mtu kimwili, kiakili, kiuchumi, kielimu, kijamii na ni kiungo kati ya mtu na mazingira yake. Shughuli za burudani ni pamoja na kupunga upepo, kusoma vitabu na magazeti, kushiriki katika michezo na sanaa za aina mbalimbali, kutalii, kuangalia televisheni, kusikiliza radio na kadhalika.

Michezo kama sehemu ya utamaduni, huwaunganisha watu kwa hiari na ni muhimu katika malezi na maisha ya kila siku ya binadamu. Mtu anayeshiriki katika michezo hujenga fikra, utii, nidhamu na moyo wa kujiamini. Burudani pia hutumika katika kutoa elimu kwa jamii, kujenga udugu na mahusiano baina ya wafanyakazi kwa wafanyakazi na baina ya nchi na nchi. Aidha, burudani ni nyenzo ya kuhimiza na kuimarisilia utendaji kazi. Hivyo:

- 6.1 MWAJIRI na CHAMA kwa pamoja wanakubaliana kwamba, ili kuleta afya bora na ukakamavu kwa Wafanyakazi na kulitangaza jina la Chuo ndani na nje ya nchi mambo yafuatayo yafanyike: -
  - 6.1.1 MWAJIRI aimarishe vikundi mbalimbali vyatia michezo na utamaduni.
  - 6.1.2 MWAJIRI aimarishe mahusiano ya kimichezo na Taasisi nyingine ili kujenga mahusiano na taasisi husika.
  - 6.1.3 Wafanyakazi wahimizwe kujishughulisha na kushiriki mazoezi ya viungo ili kujenga afya zao.
  - 6.1.4 Michezo mbalimbali iratibiwe Chuoni.
  - 6.1.5 Wafanyakazi wahamasishwe kushiriki katika michezo inayoandaliwa na Chuo
  - 6.1.6 Wafanyakazi wahamasishwe kuhusu matumizi ya lishe bora ili kujenga afya bora.

## **6.2 Matibabu na Afya ya Mtumishi**

MWAJIRI na CHAMA kwa pamoja wanakubaliana kuwa Sera ya Afya ya Chuo italenga kuboresha afya za wafanyakazi na familia zao. Hivyo: -

**6.2.1** Kila Mfanyakazi anatakiwa kuwa na Bima ya Afya Taifa (NHIF) ambalo ni takwa la kisheria kwa mujibu wa Sheria ya Bima ya Afya NA.8 ya mwaka 1999.

**6.2.2** Wafanyakazi wahamasishwe kijiunga na kutumia Mfuko wa Afya wa Jumuiya ya SUA (Mfuko wa wa ziada wa Afya wa SUA) kwa matibabu ya mtumishi husika na wategemezi wake kulingana na mwongozo wa Mfuko huo wa ziada wa Afya wa SUA;

**6.2.3** Wafanyakazi watahamasishwa kijiunga na Mfuko wa Afya wa Jumuia ya SUA kwa msingi wa hiari;

**6.2.4** Kutakuwa na mpango wa hiari wa upimaji wa afya kwa Wafanyakazi kwa kadri ya mahitaji na uwezo wa Mwajiri; na

**6.2.5** Wafanyakazi ambao wako kwenye hatari ya kuambukizwa na au kupata madhara ya vitendea kazi wanavyotumia watatakiwa kupewa vifaa kinga na kupimwa afya zao kwa kadri itakavyoshauriwa na Daktari anayetambulika na OSHA.

## **6.3 Posho na Stahili Mbalimbali za Wafanyakazi**

MWAJIRI ataendelea kutekeleza jukumu lake la kulipa posho na stahili mbalimbali za wafanyakazi pamoja na ufuatiliaji kwa kushirikiana na CHAMA. Posho na Stahili hizo ni kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zinazosimamia Utumishi wa Umma na Miongozo ya Serikali na ya Chuo (kama itakuwepo) baada ya kuidhinishwa na Serikali.

## **6.4 Mazingira Hatarishi**

MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa kutakuwa na mkakati wa kuboresha mazingira yote ya kazi ili kuondoa au kuepusha vihatarishi badala ya Wafanyakazi kulipwa posho ili waendelee kufanya kazi kwenye mazingira hayo yanayoweza kuwaathiri.

## **6.5 Posho ya Saa za Ziada**

MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa posho za aina mbalimbali zitalipwa kwa mujibu wa Miongozo ya Serikali.

## **6.6 Marupurupu ya Wastaifu**

MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa Marupurupu ya Wastaifu yatatolewa kwa mujibu wa Miongozo ya Serikali na Nyaraka za Chuo kwa kadri itakavyokuwa inarekebishwa na kuidhinishwa na Mamlaka za Serikali. Hivyo: -

**6.6.1** Mwajiri atahakikisha kuwa nyaraka kwa ajili ya stahiki za wafanyakazi wastaifu zinawasilishwa kwa taasisi husika kwa ajili ya kuwezesha malipo kufanyika kwa Wahusika.

**6.6.2** Kutakuwa na mafunzo yajulikanayo kama "Maisha baada ya Kustaafu kwa Wastaafu Watarajiwa" yatakayotolewa mapema na kugharimiwa na Mwajiri endapo hali ya fedha itaruhusu.

**6.6.3** Mwajiri na CHAMA watashirikiana kupata Watoa Mafunzo wenyewe sifa na uwezo wa kutoa mafunzo husika.

**6.7 Mavazi Rasmi na Vifaa vya Kujikinga Kazini**

MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa, Wafanyakazi wanaostahili na wanaotakiwa kuvala mavazi maalum yaani sare wawapo kazini ni; Wanasheria, Askari Polisi Wasaidizi, Wafanyakazi wa Kada za Afya, Wafanyakazi wa Miliki na Ujenzi na wafanyakazi wa Maabara. Watalipwa pesa za sare kwa utaratibu ufuatao:

- a. Wauguzi 150,000/=
- b. Madaktari wa Binadamu 100,000/=
- c. Watumishi wengine wa Taaluma za Afya 120,000/=
- d. Wafanyakazi wa Maabara, Miliki na Ujenzi 120,000/=
- e. Wanasheria 500,000/=
- f. Askari Wasaidizi 150,000/=

**6.7.1.** MWAJIRI na CHAMA watashirikiana katika kuainisha wafanyakazi wanaostahili kupata sare kwa kuzingatia vigezo na ushauri utakavyotolewa na OSHA.

**6.7.2** Wafanyakazi wanaostahili kupata mavazi maalum watapewa kwa utaratibu utakaokuwa umekubaliwa.

**6.7.3** Vifaa vya kujikinga vitanunuliwa kwa kufuata uhitaji wa wafanyakazi na eneo husika.

**6.7.4** Mavazi kwa Jumuia ya Chuo yatazingatia maadili na kama ilivyoelekezwa na Mamlaka ya Utumishi wa Umma.

**6.8 Zawadi kwa Wafanyakazi Bora**

MWAJIRI na CHAMA watashirikiana kutambua Wafanyakazi Bora kwa kutumia vigezo vya utendaji kazi pamoja na vinginevyo vinavyo halalisha sifa za Utumishi bora. Aidha, watakubaliana taratibu zitakazotumika kuhusu utoaji zawadi hizo. Zawadi zitakuwa ni kama ifuatavyo: -

- a. Mfanyakazi Bora ngazi ya Idara Tshs. 150,000/=
- b. Mfanyakazi Bora Ndaki/Kurugenzi/Shule Kuu/Taasisi/Vituo Tshs. 500,000/=
- c. Mfanyakazi Bora namba 2 kwa ngazi ya Chuo 2,000,000/=
- d. Mfanyakazi Bora namba 1 kwa ngazi ya Chuo Tshs. 3,000,000/=

**6.9 Elimu kwa Wafanyakazi**

MWAJIRI /na CHAMA wanakubaliana kuwa, Elimu kwa Wafanyakazi ni muhimu kwani itaboresha utendaji wa kazi na kuleta ufanisi. Hivyo masuala yote yahusuyo elimu yatashughulikwa kwa kuzingatia Kanuni G. (1) - (25) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009, Sera ya Mafunzo ya Chuo pamoja na miongozo yake.

**6.9.1** MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa Mwajiri atatoa punguzo katika gharama za masomo kwa Mfanyakazi/Mwenza na Mtoto wa mfanyakazi watakaopata fursa za masomo SUA kama ilivyoidhinishwa na Baraza la Chuo.

**6.9.2** Mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi yataandaliwa kutokana na mahitaji ya kipindi husika na upatikanaji wa fedha.

## **6.10 USHUGHULIKIWAJI WA VIFO**

**6.10.1** MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa MWAJIRI atagharamia mazishi ya MWAJIRIWA na/au mke/mume/mtoto/mzazi kwa kuzingatia mahitaji yaliyoordheshwa katika Kanuni Q.7 (1) - (3) ya Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma, 2009. Mwajiri atagharamia gharama zifuatazo:-

**a. Akifariki Mfanyakazi**

i. Sanduku na Sanda	-	Tshs. 400,000/=
ii. Kuchimba Kaburi	-	Tshs. 150,000/=
iii. Gharama za Kutunza Mwili	-	Tshs. 100,000/=
iv. Chakula Msibani siku 2	-	Tshs. 800,000/=
v. Usafiri akizikwa ndani ya mkoa	-	Tshs. 200,000/=
vi. Usafiri akizikwa nje ya Mkoa gharama itakokotolewa kulingana na kilometra na bei ya mafuta kwa wakati husika	-	
vii. Rambirambi ya Chuo	-	Tshs. 500,000/=

**b. Akifariki Mke/Mume/Mtoto/Mzazi wa Mfanyakazi**

i. Sanduku na Sanda	-	Tshs. 400,000
ii. Kuchimba Kaburi	-	Tshs. 150,000
iii. Gharama za kutunza mwili	-	Tshs. 100,000
iv. Chakula Msibani siku 2	-	Tshs. 800,000
v. Usafiri akizikwa ndani ya Mkoa	-	Tshs. 200,000/=
vi. Usafiri akizikwa nje ya Mkoa gharama itakokotolewa kulingana na kilometra na bei ya mafuta kwa wakati husika	-	

**6.10.2** MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa uboreshwaji wa mara kwa mara wa viwango utafanyika ili kuwezesha Wafiwa kumudu gharama za mazishi kutegemea hali ya kifedha ya MWAJIRI.

## **6.11 Uundaji wa Vyama vya Ushirika**

MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa, Wafanyakazi wataruhusiwa kuanzisha Vyama vya Ushirika na kuviendesha kwa kuzingatia Miongozo ya Serikali kupitia Msajili wa Vyama vya Ushirika.

**SEHEMU YA SABA**  
**VIMA VYA MISHAHARA NA NYONGEZA**

- 7.1 MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa, utaratibu wa mishahara kwa kila Mtumishi na nyongeza za mishahara, utazingatia cheo kilichoidhinishwa na Serikali, Miundo ya Utumishi na Nyaraka za Msajili wa Hazina na utaratibiwa na MWAJIRI kwa kufuata Miongozo ya Serikali.

**SEHEMU YA NANE  
MAPATO YATAKAYOWEZESHA KUTEKELEZA MKATABA**

- 8.1** MWAJIRI na CHAMA wamekubaliana kuwa utekelezaji wa Mkataba huu utategemea vyanzo vya mapato ambavyo vitakuwa ni tengeo kutoka mapato yanani ya Chuo kwa kila mwaka:

## SEHEMU YA TISA

### 9.1 HITIMISHO

- 9.1.2 MWAJIRI na CHAMA wanakubaliana kuwa Mkataba huu wa Hali Bora ya Wafanyakazi kazini utatumika kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia siku utakaporidhiwa. Aidha
- 9.1.3 Mkataba unaweza kufanyiwa mabadiliko wakati wowote endapo kutakuwa na matakwa ya Kisheria na uhitaji wa kimazingira wa kufanya hivyo;
- 9.1.4 Iwapo itatokea haja ya kufanya mabadiliko au kuongeza kipengele/vipengele, taarifa ya miezi mitatu itolewe kwa upande wa pili wa Wadaawa wa Mkataba huu;
- 9.1.5 Hata kama hakutakuwa na mabadiliko, bado Mkataba utasainiwa upya, ili kuondoa mkanganyiko; na
- 9.1.6 Pande zote mbili zitaheshimu Mkataba huu

MKATABA HUU UMEHITIMISHWA NA UMETIWA SAINI ZETU LEO HII SIKU YA  
TAREHE 06 MWEZI MEI 2023.

### KWA NIABA YA MWAJIRI


Jina kamili: PROFESA RAPHAEL TIHELWA CHIBUNDA

Wadhifa: MAKAMU MKUU WA CHUO

MAKAMU MKUU WA CHUO

Anuani: S. L. P. 3000 CHUO KIKUU, MOROGORO

CHUO KIKUU CHA SOKINE CHA KILIMO

Saini: ..... 

S.L.P 3000

MOROGORO, TANZANIA

### KWA NIABA YA CHAMA CHA WAFANYAKAZI RAAWU TAWI LA SUA AMBACHO NI WAKALA MAALUM WA MAJADILIANO

Jina kamili: FARAJA ESAU KAMENDU

Wadhifa: MWENYEKITI RAAWU TAWI LA SUA

Anuani: S. L. P. 3000 CHUO KIKUU, MOROGORO

Saini: 

MWENYEKITI  
RAAWU TAWI LA  
CHUO KIKUU CHA SOKINE CHA KILIMO  
S.L.P. 3000 CHUO KIKUU MOROGORO

## **SEHEMU YA KUMI**

### **REJEA**

Hati idhini ya Chuo

Sheria ya Ajira ya Mwaka 2004

Kanuni za Kudumu za Utmishi wa Umma, 2009

Kanuni za Utumishi wa Umma,2022

TPB Bank Plc and TUICO (2017). Mkataba wa Hali Bora za kazi Bainya ya TPB Bank Plc na TUICO

Yambesi, D. G. (2013). Mwongozo wa Kutayarisha na Kutekeleza Mkataba wa Huduma kwa Mteja katika Taasisi za Umma. Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dar es Salaam, Tanzania. 50pp.

PERMANENT SECRETARIAT  
PRESIDENT'S OFFICE  
PUBLIC SERVICE MANAGEMENT  
P.O.Box 670  
DODOMA